# Serikali sasa yajipanga mifugo iuzwe kwa kupimwa uzito

**Na MWANDISHI WETU,** *Dodoma*

SERIKALI inaweka utaratibu wa kuhakikisha mifugo yote inauzwa kwa kupimwa uzito, badala ya kukisia kama inavyofanyika hivi sasa katika minada na maeneo mengine.

Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa wa Dodoma, Aziza Mumba aliyasema hayo wakati akifungua mafunzo kwa wafanyabiashara na wajasiriamali wa mkoa huo yaliyoandaliwa na Wakala wa Vipimo (WMA) ili kuwawezesha kujua umuhimu wa vipimo sahihi.

Aziza aliyasema hayo alipokuwa akifungua kikao hicho kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge na kubainisha kwamba, washiriki hao wanatakiwa kuhakikisha mizani wanayotumia wale wanunuzi iko sawa.

"nazishauri mamlaka zetu za serikali za mitaa kwenye maeneo yao, kuna masoko mbalimbali yakiwemo magulio na baadhi ya minada, haina vipimo sahihi au haitumii mizani.

"Kwa hiyo tunapoendelea, serikali inaweka utaratibu kuhakikisha mifugo yote inauzwa kwa kupimwa uzito badala ya kukisia," alifafanua Mumba.

Alisema kuwa, kwa kadri wananchi watakavyozingatia suala la vipimo, manufaa yake yataonekana kwa wadau wote, anayezalisha na yule anayekwenda kutumia hiyo bidhaa, kwa kuwa atakuwa na uhakika thamani ya fedha yake inalingana na kitu kile ambacho amepewa.

Kuhusu semina hiyo, Mumba alisema itawawezesha wafanyabiashara na wenye viwanda kuelewa kwa kina suala la uzingatiaji wa vipimo sahihi.

Mbali na hayo, Mumba alisema kupitia kampeni mbalimbali, serikali imekuwa ikiendesha kaguzi ili kuhakikisha wananchi na wadau wote wanazingatia suala zima la vipimo kutokana na unyeti wake kwa maendeleo ya nchi.

Alisema wamekuwa wakipokea malalamiko kadhaa kuhusiana na matumizi batili ya vipimo kwenye mkoa huo na kupitia WMA wameendelea kushirikiana kuhakikisha wadau wote wanaendelea kutumia vipimo sahihi.

Mumba alifafanua kuwa, Dodoma peke yake kuna viwanda zaidi ya 3,000, vikiwemo vya kusindika alizeti, unga, viwanda vya mvinyo, hivyo suala la kuzingatia vipimo ni muhimu kuanzia shambani wakulima wanapokuwa wanapouza mazao.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa WMA, Stella Kahwa, alisema WMA jukumu lake kuu ni kumlinda mlaji kupitia matumizi sahihi ya vipimo, hivyo wana kazi ya kuhakiki vipimo na kuhakikisha vinatumika kwa usahihi.

Pia, wana jukumu la kuhakikisha bidhaa zinazozalishwa na viwanda nchini zinafungashwa kwa usahihi, kwa sababu ili uweze kupenya kwenye soko la kimataifa ni lazima ufungashaji wa bidhaa zako uzingatie miongozo yote ya Shirika la Vipimo Duniani," alisema Kahwa.

Alisema WMA ni mwanachama hai wa Shirika la Vipimo Duniani, hivyo wao wanatakiwa kutoa miongozo hiyo kwa wazalishaji wa ndani ili waweze kushindana kimataifa na kitaifa.

Alisema ili kuelekea Tanzania ya Viwanda, lazima vipimo sahihi vizingatiwe na kwamba wanafanya semina za aina hiyo nchini kote ili kuwafikia wafungashaji na wazalishaji wadogo wadogo waweze kukua, wawe wazalishaji na wafungashaji wa kati na mwisho wa siku wawe wa kimataifa.

Naye Kaimu Meneja wa WMA, Mkoa wa Dodoma, Karim Zuberi, alisema semina hiyo ni kwa ajili ya kuelimisha matumizi sahihi ya vipimo na ufungaji kwa wafanyabiashara na wajasiriamali mbalimbali wenye viwanda na wengineo.

Alisema semina hiyo ni mwendelezo wa semina za mara kwa mara ambazo wamekuwa wakizifanya ambapo wanapokuwa maeneo ya uzalishaji wanatoa elimu kwa mfanyabiashara mwenye kiwanda mmoja mmoja na kwa watumishi wa Serikali na wamekuwa wakishirikiana na watendaji wa Kata.

Washiriki wa mafunzo hayo waliahidi kuzingatia mafunzo hayo na kuyatumia katika shughuli zao huku wakisema hata walaji watakuwa na uhakika na kile walichopimiwa na wameahidi kuwa walimu.

Mwenyekiti wa Kikundi cha Wanawake Wapambana Mkoa wa Dodoma, Asuna Baya, alishukuru kwa mafunzo hayo kwamba yatawasaidia kwenye shughuli zao.

**MATUMIZI**

Kwa kadri wananchi watakavyozingatia suala la vipimo, manufaa yake yataonekana kwa wadau wote.

UHURU · UK · 16, 6 MEI, 2021

# Mifugo yote kuuzwa kwa kupimwa uzito

Na Mwandishi Wetu, Dodoma

SERIKALI inaweka utaratibu wa kuhakikisha mifugo yote inauzwa kwa kupimwa uzito, badala ya kukisia kama inavyofanyika sasa kwenye minada na maeneo mengine nchini.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa wa Dodoma, Aziza Mumba, wakati akifungua mafunzo ya wafanyabiashara na wajasiriamali wa mkoa huo yaliyoandaliwa na Wakala wa Vipimo (WMA) ili kuwawezesha kujua matumizi sahihi ya vipimo na ufungashaji.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dkt. Binilith Mahenge, Mumba alisema wafanyabiashara na wajasiriamali wanatakiwa kuhakiki mizani wanayotumia kwenye manunuzi ili iwe sawa.

"Kwa hiyo nazishauri mamlaka zetu za Serikali za Mitaa kwenye maeneo yao kuna masoko mbalimbali yakiwemo magulio na baadhi ya minada, haina vipimo sahihi au haitumii mizani, kwa hiyo tunapoendelea Serikali inaweka utaratibu kuhakikisha mifugo yote inauzwa kwa kupimwa uzito badala ya kukisia," alifafanua Mumba.

Alisema kwamba kwa kadri wananchi watakavyozingatia suala la vipimo, manufaa yake yataonekana kwa wadau wote, anayezalisha na yule anayekwenda kutumia hiyo bidhaa, kwani atakuwa na uhakika kwamba thamani ya fedha yake inalingana na kitu kile ambacho amepewa.

"Hicho ndicho kikubwa zaidi, kwani pande zote zinafaidika na matumizi sahihi ya vipimo," alisema Mumba.

Alisema semina hiyo itawezesha wafanyabiashara na wenye viwanda kuweza kuelewa kwa kina suala la uzingatiaji wa vipimo sahihi.

Kwa mujibu wa Mumba kupitia kampeni mbalimbali, Serikali imekuwa ikiendesha kaguzi ili kuhakikisha wananchi na wadau wote wanazingatia suala zima la vipimo kutokana na unyeti wake katika maendeleo ya nchi yetu.

Aliongeza kwamba wamekuwa wakipokea malalamiko kadhaa kuhusiana na matumizi batili ya vipimo kwenye mkoa huo na kupitia WMA, wameendelea kushirikiana kuhakikisha wadau wote wanaendelea kutumia vipimo sahihi.

Alizidi kufafanua kwamba Dodoma peke yake kuna viwanda zaidi ya 3,000, vikiwemo vya kusindika alizeti, unga, viwanda vya mvinyo, hivyo suala la kuzingatia vipimo ni muhimu sana kuanzia shambani wakulima wanapokuwa wanauza mazao.

Kwa upande wake Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa WMA, Stella Kahwa, alisema WMA jukumu lake kuu ni kumlinda mlaji kupitia matumizi sahihi ya vipimo.

"Kwa hiyo tuna kazi ya kuhakiki vipimo na kuhakikisha vinatumika kwa usahihi," alisema na kuongeza; "Tuna jukumu la kuhakikisha kwamba bidhaa zinazozalishwa na viwanda vyetu zinafungashwa kwa usahihi, kwa sababu ili uweze kupenya kwenye soko la kimataifa ni lazima ufungashaji wa bidhaa zako uzingatie miongozo yote ya Shirika la Vipimo Duniani," alisema Kahwa.

Alisema WMA ni mwanachama hai wa Shirika la Vipimo Duniani, hivyo wao wanatakiwa kutoa miongozo hiyo kwa wazalishaji wa ndani ili waweze kushindana kimataifa na kitaifa.

Aliongeza kwamba ili kuelekea Tanzania ya Viwanda , lazima vipimo sahihi vizingatiwe na kwamba wanafanya semina za aina hiyo nchini kote ili kuwafikia wafungashaji na wazalishaji wadogo wadogo waweze kukua, wawe wazalishaji na wafungashaji wa kati na mwisho wa siku wawe wa kimataifa.

"Kwa hiyo tunatumia semina hizi kwa ajili ya kuwaelimisha wafungashaji na wazalishaji wa bidhaa mbalimbali nchini na sasa tupo mkoa wa Dodoma na mikoa mingine zimekwisha fanyika semina na mafunzo kama haya kwa ajili ya kujenga uchumi wa viwanda Tanzania," alisema Kahwa.

Naye Kaimu Meneja wa WMA mkoa wa Dodoma, Karim Zuberi, alisema semina hiyo ni kwa ajili ya kuelimisha matumizi sahihi ya vipimo na ufungaji kwa wafanyabiashara na wajasiriamali mbalimbali wenye viwanda na wengineo.

Alisema semina hiyo ni mwendelezo wa semina za mara kwa mara ambazo wamekuwa wakizifanya ambapo wanapokuwa maeneo ya uzalishaji wanatoa elimu kwa mfanyabiashara mwenye kiwanda mmoja mmoja na kwa watumishi wa Serikali na wamekuwa wakishirikiana na watendaji wa Kata.

Zuberi alisema wao kama mkoa ni kuhakikisha Dodoma inaondokana na matumizi yasiyokuwa sahihi ya vipimo.

Alisema watakuwa wanafanya kaguzi mbalimbali zikiwemo za kawaida na za kushtukiza. Zuberi alisema kwa sasa vipimo vimeongezeka na wanakagua vipimo vingi, hivyo hali ni nzuri.

Washiriki wa mafunzo hayo waliahidi kuzingatia mafunzo hayo na kuyatumia katika shughuli zao. Walisema hata walaji watakuwa na uhakika na kile walichopimiwa na wameahidi kuwa walimu kwa wengine ambao hawakupata fursa ya kushiriki mafunzo hayo.

Naye Mwenyekiti wa Kikundi cha Wanawake Wapambana Mkoa wa Dodoma, Asuna Baya, alishukuru kupatiwa mafunzo hayo na kwamba yatawasaidia kwenye shughuli zao.

Aliipongeza WMA kwa kuwapatia mafunzo hayo na kwamba yatawasaidia kubadilika na kuwa na nidhamu ya vipimo kwa kuondokana na vipimo vya mazoea. Alisema Dodoma sasa hivi ni makao makuu, hivyo kuna haja ya kuzingatia vipimo wanavyoelimishwa na ili kufanikiwa hilo ni lazima wawe na hofu ya Mungu.



## Rais Samia ateta na Mjumbe Maalum wa Katibu Mkuu UN

Na Mwandishi Wetu, Nairobi

RAIS Samia Suluhu Hassan, amekutana na kufanya mazungumzo na Mjumbe Maalum wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa katika Ukanda wa Maziwa

Scanned with CamScanner

NIPASHE 9, MEI 6, 2021



# Mifugo sasa kupimwa uzito kabla ya kuuzwa

**Na Mwandishi Wetu**, DODOMA

SERIKALI inaweka utaratibu wa kuhakikisha mifugo yote inauzwa kwa kupimwa uzito badala ya kukisia kama inavyofanyika sasa kwenye minada na maeneo mengine.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa wa Dodoma, Aziza Mumba wakati akifungua mafunzo ya kwa wafanyabiashara na wajasiriamali wa mkoa huo yaliyoandaliwa na Wakala wa Vipimo (WMA) ili kuwawezesha kujua umuhimu wa vipimo sahihi.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, Mumba alisema wanatakiwa kuhakikisha minzani wanayotumia wale wanunuzi iko sawa.

"Kwa hiyo naishauri mamlaka zetu za Serikali za Mitaa kwenye maeneo yao kuna masoko mbalimbali yakiwamo magulio na baadhi ya minada, haina vipimo sahihi au haitumii mizani, kwa hiyo tunapoendelea Serikali inaweka utaratibu kuhakikisha mifugo yote inauzwa kwa kupimwa uzito badala ya kukisia," alifafanua Mumba.

Alisema kwa kadri wananchi watakavyozingatia suala la vipimo, manufaa yake yataonekana kwa wadau wote, anayezalisha na yule anayekwenda kutumia hiyo bidhaa, kwani atakuwa na uhakika kwamba thamani ya fedha yake inalingana na kitu kile ambacho amepewa.

"Hicho ndicho kikubwa zaidi kwani pande zote zinafaidika na matumizi sahihi ya vipimo," alisema Mumba.

Alisema semina hiyo itawezesha wafanyabiashara na wenye viwanda kuweza kuelewa kwa kina suala la uzingatiaji wa vipimo sahihi.

Kwa mujibu wa Mumba, kupitia kampeni mbalimbali, Serikali imekuwa ikiendesha kaguzi ili kuhakikisha wananchi na wadau wote wanazingatia suala zima la vipimo kutokana na unyeti wake katika maendeleo ya nchi yetu.

Aliongeza kwamba wamekuwa wakipokea malalamiko kadhaa kuhusiana na matumizi batili ya vipimo kwenye mkoa huo na kupitia WMA, wameendelea kushirikiana kuhakikisha wadau wote wanaendelea kutumia vipimo sahihi.

Alifafanua zaidi kwamba Dodoma peke yake kuna viwanda zaidi ya 3,000, vikiwamo vya kusindika alizeti, unga, viwanda vya mvinyo, hivyo suala la kuzingatia vipimo ni muhimu sana kuanzia shambani wakulima wanapokuwa wanapouza mazao.

Kwa upande wake Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa WMA, Stella Kahwa, alisema WMA jukumu lake kuu ni kumlinda mlaji kupitia matumizi sahihi ya vipimo.

"Kwa hiyo tuna kazi ya kuhakiki vipimo na kuhakikisha vinatumika kwa usahihi," alisema na kuongeza;

"Tuna jukumu la kuhakikisha kwamba bidhaa zinazozalishwa na viwanda vyetu zinafungashwa kwa usahihi, kwa sababu ili uweze kupenya kwenye soko la kimataifa ni lazima ufungashaji wa bidhaa zako uzingatie miongozo yote ya Shirika la Vipimo Duniani."

Alisema WMA ni mwanachama hai wa Shirika la Vipimo Duniani, hivyo wao wanatakiwa kutoa miongozo hiyo kwa wazalishaji wa ndani ili waweze kushindana kimataifa na kitaifa.

Aliongeza kwamba ili kuelekea Tanzania ya Viwanda , lazima vipimo sahihi vizingatiwe na kwamba wanafanya semina za aina hiyo nchini kote ili kuwafikia wafungashaji na wazalishaji wadogo wadogo ili waweze kukua, wawe wazalishaji na wafungashaji wa kati na mwisho wa siku wawe wa kimataifa.

"Kwa hiyo tunatumia semina hizi kwa ajili ya kuwaelimisha wafungashaji na wazalishaji wa bidhaa mbalimbali nchini na sasa tupo Mkoa wa Dodoma na mikoa mingine zimekwisha fanyika semina na mafunzo kama haya kwa ajili ya kujenga uchumi wa viwanda Tanzania," alisema Kahwa.

Naye Kaimu Meneja wa WMA Mkoa wa Dodoma, Karim Zuberi, alisema semina hiyo ni kwa ajili ya kuelimisha matumizi sahihi ya vipimo na ufungaji kwa wafanyabiashara na wajasiriamali mbalimbali wenye viwanda na wengineo.

Scanned with CamScanner